

YALIYOMO

| | |
|-------------------------------------------------------------------|-----|
| 1 ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMI..... | III |
| 2 MAELEZO YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA | IV |
| 3 MAELEZO YA MKURUGENZI MTENDAJI..... | V |
| 4 UTANGULIZI | VI |
| 5 MUUNDO WA MPANGO..... | VII |
| SURA YA KWANZA: UTANGULIZI..... | 1 |
| 1.1 HISTORIA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO..... | 1 |
| 1.2 WASIFU WA WILAYA..... | 2 |
| 1.3 IDADI YA WATU..... | 2 |
| 1.4 MAGONJWA 10 YANAYOWASUMBUA WANANCHI WILAYANI | 2 |
| 1.5 VVU NA UKIMWI | 2 |
| 1.6 MAWASILIANO | 3 |
| 1.7 WAJIBU WA HALMASHAURI YA WILAYA | 3 |
| 1.7.1 Dira ya Halmashauri: | 3 |
| 1.7.2 Dhima ya Halmashauri:..... | 3 |
| 1.7.3 Misingi Bora ya Utendaji Kazi; | 3 |
| 1.8 MALENGO YA KIUTENDAJI..... | 4 |
| 1.9 METHODOLOGIA ILIYOTUMIKA | 5 |
| SURA YA PILI: UCHAMBUZI WA HALI HALISI | 6 |
| 2.1 UTANGULIZI | 6 |
| 2.2 MALENGO YA HALMASHAURI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE: | 7 |
| 2.3 MALENGO YALIYOPANGWA NA SHABAHA..... | 7 |
| 2.4 UCHUNGUZI WA TAASISI | 12 |
| 2.5 CHANGAMOTO KWA UJUMLA ZINAZOKABILI HALMASHAURI..... | 16 |
| SURA YA TATU: MAPITIO YA UTEKELEZAJI..... | 18 |
| 3.1 MAPITIO..... | 18 |
| SURA YA NNE: MPANGO MKAKATI WA MWAKA 2016/2017 - 2020/2021..... | 24 |
| 4.1. UTANGULIZI | 24 |
| 4.1.1 Dira ya Halmashauri: | 24 |
| 4.1.2 Dhima ya Halmashauri:..... | 24 |
| 4.1.3 Misingi Bora ya Utendaji Kazi; | 24 |
| SURA YA TANO: MPANGILIO WA MATOKEO YA KAZI | 33 |
| 5.1 UTANGULIZI | 33 |
| 5.2 UHUSIANO NA MPANGO WA TAIFA WA MIAKA MITANO..... | 33 |
| SURA YA SITA: UFUATILIAJI, MAPITIO NA TATHMINI | 36 |

| | |
|---------------------------------------------|----|
| 6.1 UTANGULIZI | 36 |
| 6.2 MAPITIO NA TATHMINI YA NUSU MWAKA | 36 |

1 ORODHA YA VIFUPISHO.

| | |
|-----------------|----------------------------------------------------------|
| ARV | Dawa za kupunguza makali ya UKIMWI |
| CBOs | Mashirika ya Kijamii |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| DPs | Washirika wa Maendeleo |
| FBOs | Mashirika ya Dini |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| ITV | Kituo cha Televisheni |
| KPIs | Viashiria vikuu vya utendaji |
| LGAs | Mamlaka za Serikali za mitaa |
| MDAs | Wizara, idara na mawakala |
| MIS | Mfumo wa usimamizi wa Taarifa |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| NGOs | Mashirika yasiyo ya kiserikali |
| NMB | Benki ya Taifa ya Makabwela |
| O&OD | Fursa na vikwazo vya maendeleo |
| PMO | Prime Minister's Office |
| PMU | Kitengo cha manunuzi |
| SACCOS | Chama cha kuweka na kukopa |
| SWOC | Uimara, udhaifu, fursa, na changamoto. |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TBC | Shirika la utangazaji Tanzania |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VVU | Virusi Vya Ukimwi |

2 MAELEZO YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA.

Halmashauri kwa kushirikiana na jamii imeandaa wasifu wa miaka mitano wa Halmashauri kama dira ya kufikia malengo iliyojiwekea. Halmashauri ilibainisha vipaumbele vilivyopatikana kupitia mbinu shirikishi ambapo jamii ilihusika moja kwa moja katika uibuaji wa vipaumbele hivyo. Mbinu shirikishi inawezesha jamii kuwa na umiliki wa miradi iliyoibuliwa, miradi kuwa endelevu na pia jamii kuwa na maendeleo endelevu kwa ujumla.

Maeneo ya vipaumbele yaliyoibuliwa na jamii katika Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2016/17 - 2020/21) ni Elimu, Afya, Maji, Miundombinu, Biashara na Uwekezaji Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Utalii. Hivyo basi mpango na bajeti hii umeandaliwa kulingana na Sera za Taifa za Kisekta, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (NFYDP 2016/17 - 2020/21), Maono ya Maendeleo Tanzania (TDV 2025) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015.

Ili kufikia malengo tarajiwa, wadau wote wakiwemo Madiwani, Jamii, Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na Washirika wa Maendeleo sharti wahusike kikamilifu katika kutekeleza wajibu wao. Ni matumaini yangu kuwa, utekelezaji wa mpango na bajeti hii kwa mwaka 2016/2017 utachochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wana Kalambo.



Mh: Daud N. Sichone
**MWENYEKITI WA HALMASHAURI
KALAMBO**

3 MAELEZO YA MKURUGENZI MTENDAJI

Mpango wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kwa mwaka 2016/17 hadi 2020/21 umeakisi vipaumbele vya Halmashauri na Taifa kwa ujumla katika miaka mitano ijayo. Mpango huu umefungamana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2016/17-2020/21, Sera za Taifa za Kisekta, Maono ya Maendeleo Tanzania (TDV 2025) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015.

Wajibu mkubwa wa Halmashauri ni kuleta maendeleo katika mamlaka za chini za utawala na jamii nzima ya Kalambo ili kufikia malengo na shabaha tuliyojiwekea katika kuleta maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Haya yote yatawezekana kupitia uwepo wa Amani na utulivu, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuwajengea jamii uwezo.

Mpango huu unalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Halmashauri ya wilaya ya Kalambo kama taasisi ya serikali katika kuwezesha na kusaidia jamii kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na ufasaha katika kutoa huduma na kutumia rasirimali zilizopo katika kuongeza maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mpango huu umeunganisha shughuli/miradi yote ya maendeleo na ya kila siku.

Mpango umeandaliwa ili kuongeza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia uratibu mzuri na kutumia kanuni za utawala bora na kuwezesha jamii kushiriki na kupata huduma bora ili kuleta usawa wa kijamii na kiuchumi katika jamii kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa mpango huu utaleta ufanisi katika utendaji kazi wa kila mdau na kuchochea maendeleo endelevu ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla.

Eng. Simon Ngagani
Mkurugenzi wa Halmashauri
KALAMBO

4 UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo wa Wilaya umeundwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2016/17 hadi 2020/21. Mpango unafafanua Dhima, Dira, mambo ya msingi, malengo, shabaha na viashiria vya utendaji ambayo yamepatikana kutokana na uchambuzi wa wadau wa maendeleo waliopo wilayani, udhaifu, uimara, fursa na vikwazo, kujitathmini na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mpango unaanza kwa kufafanua hali halisi ambayo inatoa mtazamo wa kiutendaji katika Halmashauri ya wilaya ambao unatoa mkakati mbadala. Mpango umezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka 5 (FYNDP 2016/17 - 2020/21), Maono ya Maendeleo Tanzania (TDV 2025) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 ambapo mambo ya msingi yanayohitaji utekelezaji wa kina yamepatikana, ambayo ni;

- (i) Maendeleo ya Kilimo
- (ii) Maendeleo ya Biashara na Uwekezaji
- (iii) Maendeleo ya Miundombinu
- (iv) Kuboresha Huduma za Jamii
- (v) Kuboresha utalii
- (vi) Usimamizi wa Mazingira

Ili kuondoa changamoto kubwa zilizopo na kuimarisha utendaji wenye matokeo chanya, malengo yafuatayo yamebainishwa kama ifuatavyo;

- i. Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI na kuimarisha huduma wezeshi kwa waathirika.
- ii. Kuongeza, kuendeleza, na kutekeleza kwa ufanisi mpango wa Taifa wa kuzuia Rushwa (National Anti-corruption Program).
- iii. Kuimarisha uwezo wa wilaya kutekeleza majukumu yake ya kisheria.
- iv. Kuimarisha huduma za kiuchumi na kimiundombinu
- v. Kuimarisha huduma bora za jamii
- vi. Kuimarisha utawala bora na huduma za kiutawala

5 MUUNDO WA MPANGO MKAKATI.

Mpango huu umepangwa katika sura sita: Sura ya kwanza imeelezea utangulizi, ambapo historia na wasifu wa wilaya umeelezewa. Pia imefafanua hali za kisékta za halmashauri, imefafanua udhaifu, uimara, fursa na vikwazo, kujitathmini na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku na methodolojia. Katika sura ya pili mpango umejadili kwa kina kuhusu uchambuzi wa mtazamo wa muda mrefu wa kitaasisi. Sura ya tatu imejadili Malengo na Viashiria vya Mpango wa Maendeleo utakaopimwa baada ya miaka mitano. Sura ya nne imejadili kuhusu rasilimali fedha inayohitajika kwa ajili ya kutekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano 2016/17 - 2020/21. Sura ya tano inaonesha ufafanuzi wa kina kupitia jedwali la Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (FYDP Matrix). Na mwisho sura ya sita inajadili kwa kina ufuatiliaji (Monitoring) na tathmini (evaluation) ya malengo ya kimkakati ya wilaya.

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Historia ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo

Halmashauri ya wilaya ya Kalambo ni miongoni mwa wilaya 176 za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ni miongoni mwa wilaya nne (4) za Mkoa wa Rukwa. Makao makuu ya wilaya yapo katika mji wa Matai. Kalambo kunapatikana pia mapalomoko ya maji ya Kalambo (Kalambo Falls), ambayo ni mapalomoko marefu na yenye kina kirefu katika bara la Afrika. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo inakadiriwa kuwa katika nyuzi za Latitudo 8.15 na 32.1 Kusini mwa Ikweta, na Longitudo 31 na 32.1 Mashariki ya Greeniwichi; Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo inapatikana Meta 1,700 juu ya usawa wa Bahari. Halmashauri imepakana na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga upande wa Mashariki, nchi ya Zambia kwa upande wa Kusini, Halmashauri ya Wilaya ya Momba upande wa Kusini - mashariki, ziwa Tanganyika upande wa Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi upande wa Kaskazini- Magharibi na Manispaa ya Sumbawanga upande wa Kaskazini. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ilimegwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga tarehe 23, Desemba, 2012, kwa tangazo la Serikali GN 631.

Shughuli kuu ya Halmashauri ni kuwezesha maendeleo na ustawi wa ngazi za chini za utawala katika kutekeleza na kufika dira na shabaha ya Serikali za mitaa hususani mamlaka za chini za utawala (kata, vijiji na mitaa) kwa kulenga dira ya Taifa ya maendeleo. Hii itawezekana kwa kutoa huduma za ushauri na kuwezesha mtiririko wa taarifa, maagizo na maelekezo, miongozo, sera, sheria na fedha za Serikali.

1.2 Wasifu wa Wilaya

Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo inakadiriwa kuwa na jumla ya eneo la ekari 1,165,101 ambapo ekari 124,541 ni maji (10.69%) na ekari 1,040,560 ni ardhi (89.31%). Kiutawala, Halmashauri ina tarafa 5 ambazo ni Matai, Kasanga, Mwimbi, Mambwe Nkoswe na Mwazye. Halmashauri imegawanyika katika kata 23 ambazo ni Kasanga, Mkowe, Msanzi, Matai, Sopa, Mwazye, Katazi, Mwimbi, Mambwekenya, Mambwenkoswe, Legezamwendo, Ulumi, Mnamba, Katete, Kisumba, Mkali, Kileshe, Sundu, Lyowa, Mpombwe, Mbuluma, Kanyezi na Samazi. Halmashauri ina vijiji 111.

1.3 Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwezi agost, 2012 According to Census of housing and population, conducted in August, 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ina jumla ya watu wapatao 207,700 ambapo 107,226 ni wanawake na 100,474 ni wanaume. Mwaka 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao 238,760 ambapo 123,261 walikuwa wanawake na 115,499 wanaume. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ina vitongoji 439 na kaya 47,752.

1.4 Magonjwa 10 yanayowasumbua wananchi wilayani

Malaria, VVU na UKIMWI, Shinikizo la Damu, Kisukari, Kifua Kikuu, Kichomi, Kansa, Minyoo ya tumbo, Kuharisha na magonjwa ya ngozi and Skin infections.

1.5 VVU na UKIMWI

Mwaka 2015, VVU na UKIMWI katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ulishuka kutoka 2.4% 2015 hadi 1.6% mwaka 2016.

1.6 Mawasiliano

Halmashauri inahudumiwa na huduma za mawasiliano za makampuni binafsi ya simu za mkononi (Vodacom, Tigo, airtel, na halotel) ambapo mitandao hiyo inapatikana katika vituo vyote na maeneo mengi ya vijijini. Licha ya huduma za redio na televisheni zinazopatikana sehemu kubwa ya nchi zinazotolewa na shirika la utangazaji Tanzania (TBC) na Televisheni ya ITV na televisheni nyingine, lakini pia kuna vituo vya utangazaji vya redio kwa masafa ya FM vya Chemichemi na Ndingara zinazosikika maeneo machache.

1.7 Wajibu wa Halmashauri ya Wilaya

Halmashauri imetoa mwongozo wa shughuli za msingi zinazotakiwa kutekelezwa katika Waraka Namba 7 wa Serikali za mitaa wa mwaka 1982. Hivyo kwa mujibu wa sheria, wajibu wa msingi wa Halmashauri ni kuhakikisha utoaji wa huduma bora za kijamii na kiuchumi zenye kiwango na pia kuhakikisha Amani na utulivu vinakuwepo katika jamii kwa kuwezesha mazingira ya kata na vijiji kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

1.7.1 Dira ya Halmashauri:

“Dira ya Halmashauri ni, Kuwa na jamii yenye maisha bora na kutoa huduma bora kwa wakati”

1.7.2 Dhima ya Halmashauri:

“Kuhakikisha tunatumia kwa kiwango cha juu rasilimali zilizopo, ili kuboresha maisha ya jamii na kuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.”

1.7.3 Misingi Bora ya Utendaji Kazi;

- **Bidii**

Kufanya kazi kwa ujuzi, ufasaha na ufanisi lakini kwa kuzingatia viwango vya juu vya nidhamu.

- **Ushirikiano**

Kufanya kazi kama timu, kushirikiana ujuzi, taarifa na ujuzi ili kufikia malengo ya maendeleo tuliyojiwekea.

- **Utawala bora**

Kuweka jitihada katika kukidhi matazamio au mahitaji ya mteja.

- **Uadilifu**

Kuzingatia maadili katika kutoa huduma kwa wateja/jamii.

- **Uwajibikaji**

Kuwajibika kutoa huduma kwa jamii kwa wakati bila urasimu.

- **Heshima**

Kusikiliza na kuhudumia kwa nidhamu.

- **Ushirikishwaji**

Kushirikisha wadau wengi iwezekanavyo katika kufanya maamuzi na utekelezaji.

1.8 Malengo ya Kiutendaji

Mpango wa maendeleo wa 2015/16 - 2020/21 umeundwa kwa kuzingatia malengo ya kimkakati kama ilivyoielezwa hapa chini;

- Kuimarisha huduma za afya na kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI
- Kuimarisha, kuendeleza na kutekeleza kwa ufanisi sera ya Taifa ya kupambana na Rushwa.
- Kuimarisha upatikanaji, usawa na ubora wa huduma za jamii.
- Kuongeza idadi na ubora wa huduma za kijamii, kiuchumi na kimiundombinu.
- Kuboresha utawala bora na huduma za kiutawala.
- Kuimarisha ustawi wa jamii, jinsia na kuwajengea wananchi uwezo.

- Kuimarisha usimamizi wa dharula na majanga mbalimbali.

1.9 Methodologia Iliyotumika

Mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano umeundwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa muda mrefu na Mwongozo wa Bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mpango wa pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP II 2016/17 – 2020/21). Mpango huu pia umeandaliwa kwa kutumia njia shirikishi ya fursa na Vikwazo (O&OD) kwa kutumia maafisa na uongozi wa Halmashauri ya wilaya. Rejea ilifanyika kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo Tanzania (TDV 2025). Ilani ya uchaguzi ya chama tawala (CCM 2015), Sera za Kisekta na Rekebisho la Programu ya Utumishi wa Umma Awamu ya Pili (PSRP II).

Katika kuandaa mpango huu, shughuli zifuatazo zilifanyika:

- Tathmini ya utendaji (Performance Review) kwa Mwaka, 2013, 2014 and 2015.
- Uchambuzi wa hali halisi (Situational analysis), ambapo mambo ya msingi, Uimara, Udhaifu, Fursa na Vikwazo (SWOC) vilizingatiwa.
- Kutafakari dira, dhima na misingi ya utendaji (core values)
- Tafakari ya malengo, mikakati, shabaha na viashiria vya msingi vya utendaji.

SURA YA PILI: UCHAMBUZI WA HALI HALISI

2.1 Utangulizi

Sura hii imeiangalia Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kati ya mwaka 2012/13 hadi 2015/16. Mpangilio umeangalia mamlaka ya Halmashauri kama ilivyoelekezwa katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) kwa sheria Na. 7 ya 1982 iliyorekebishwa; ambapo Wajibu na kazi, dira na dhima, tathmini ya utendaji katika mafanikio, changamoto, na utatuzi katika kila lengo umezingatiwa.

Sura hii pia inatoa muhtasari wa matokeo ya wadau wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. Uchambuzi unaonesha matarajio na huduma ambayo jamii inatarajia kupata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na mwisho ni uchambuzi wa SWOC ambao unatoa taswira ya Halmashauri.

Kupitia tathmini ya taasisi maeneo ya kufanyiwa marekebisho yalibainishwa kama maeneo ya msingi ili yafanyiwe marekebisho katika mpango ujao.

Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo

Serikali ilianzisha Serikali za mitaa (Mamlaka za Wilaya) kwa Sheria Namba 7 ya 1982 na marekebisho ambayo yalinuia kuimarisha mfumo wa Serikali za mitaa kwa kupeleka madaraka katika Serikali za mitaa (D by D)

Hivyo, mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kama ilivyoelezewa katika sharia hiyo ni kuwezesha na kuendeleza Amani, miongozo, na utawala bora katika maeneo yake, kuimarisha ustawi wa jamii na ustawi wa kiuchumi wa watu wote katika Halmashauri, kuzingatia sera na mipango ya Taifa ya maendeleo ya miji na vijiji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya watu wa Halmashauri.

Halmashauri ina wajibu kuchukua hatua za dhati katika kutokomeza uhalifu na kuhakikisha Amani na utulivu na udhibiti wa mali za umma na binafsi zinalindwa kisheria; ili kuwa na udhibiti na kuinua kilimo, biashara, biashara za kimataifa na viwanda; ili kuwa na afya bora, elimu na jamii, utamaduni na ustawi wa watu; ili kupunguza umasikini na ufukara, na kwa msaada na kuboresha maisha ya vijana, wazee, walemavu na wasiojiweza, na kwa maendeleo, uhamasishaji na kuwekeza nguvu katika uzalishaji ili kupambana na maadui watatu ambao ni umasikini, maradhi na ujinga.

2.2 Malengo ya Halmashauri Katika Kutekeleza Majukumu Yake:

Ni kuwa na matokeo mazuri kutokana na ugatuaji wa madaraka katika masuala ya siasa, kifedha na kiutawala yanayohusiana na shughuli, utawala, wajibu na huduma katika ngazi zote za utawala katika halmashauri; kukuza na kuhakikisha ushiriki wa kidemokrasia wa watu wote katika kufanya maamuzi, na kuanzisha na kusimamia vyanzo vinavyokubalika vya mapato na rasilimali nyingine ili kuiwezesha Halmashauri kufanya shughuli mbalimbali kwa ufanisi na kuongeza uwajibikaji katika masuala ya fedha katika Halmashauri, washirika wake na watumishi wote kwa ujumla.

2.3 Malengo Yaliyopangwa na Shabaha.

Katika kipindi cha 2016/17 - 2020/21, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo itatumia maeneo muhimu ya matokeo ambayo yatapimwa kila mwaka wa fedha kama ifuatavyo;

Lengo A: Kuboresha Huduma na Kupunguza Maambukizi ya VVU /UKIMWI:

Malengo mahsusi yaliyopangwa

- Kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU miongoni mwa watumishi wa Halmashauri ifikapo Juni, 2021.
- Kutoa chakula bora chenye virutubisho kwa watu wanaoishi katika makundi magumu kutoka makundi 74 hadi 110 ifikapo Juni, 2021.
- Kutoa mafunzo ya ufahamu na ujuzi kuhusu kuosha mikono na udhibiti wa VVU/UKIMWI katika vijiji 25 ifikapo Juni, 2021.
- 80% ya jamii katika Halmashauri ifikiwe na elimu bora ya afya ifikapo Juni, 2021.
- Ushirikiano katika shughuli na vifaa tiba katika kupambana na VVU na kifua kikuu kuongezeka kutoka shughuli 30 hadi 60 ifikapo Juni, 2021.
- 70% ya wagonjwa wa TB wanabainika na kupewa matibabu sahihi katika vituo vya afya na zahanati na pia wakiwa katika jamii ifikapo Juni, 2021.
- 60% ya wagonjwa wanaopata dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARV) wazingatie ratiba ya matibabu, na kuhakikisha huduma za dawa za ARV na vipimo vya maabara zinapatikana ifikapo Juni, 2021.
- 80% ya magonjwa ya homa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) wapate huduma sahihi ya matibabu ndani ya saa 24 maara dalili zinapoonekana ifikapo Juni, 2021.

Lengo B: Utekelezaji Makini wa Mkakati wa Kupambana na Kuzuia Rushwa.

Malengo mahsusi yaliyopangwa

- Watumishi wa Halmashauri kujengewa uwezo katika kupambana na rushwa ndogondogo na rushwa kubwa ifikapo Juni, 2021.

- Watumishi 59 wa vituo vya afya kujengewa uwezo katika kupambana na rushwa ndogondogo na rushwa kubwa ifikapo Juni, 2021.
- Kufanya semina ya mwaka ya watumishi wa Halmashauri juu ya namna ya kupambana na rushwa kwa kushirikiana na TAKUKURU ifikapo Juni, 2021.
- Masanduku ya maoni kutumika ipasavyo ifikapo Juni, 2021.

Lengo C: Kuboresha Upatikanaji na Utoaji wa Huduma Bora na Utoaji wa Huduma Bora za Kijamii na Kiuchumi
Malengo Mahususi Yaliyopangwa

- Kuongeza uanzishwaji wa elimu ya awali katika kila shule ya msingi ifikapo Juni, 2021.
- Kuandikisha wanafunzi wa elimu ya awali wenye umri wa miaka 5 hadi 6 kwa asilimia mia moja (100%) ifikapo Juni, 2021.
- Kuongeza stahiki za walimu wa elimu ya msingi katika shule zote za msingi ifikapo Juni, 2021.
- Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuongeza kiwango cha ufauru katika mitihani ya kitaifa ifikapo Juni, 2021.
- Kuongeza idadi ya majengo na samani za shule za Sekondari ifikapo Juni, 2021. .
- Kutoa chanjo ya kinga kuongezeka kutoka 90% hadi 95% kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano ifikapo Juni, 2021.
- 100% ya vituo vya afya na zahanati kuwa na madawa yakutosha kwa ajili ya tiba ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukizwa ifikapo Juni, 2021.
- 100% ya jamii wafikiwe na jumbe zenye elimu muhimu na sahihi za

afya ifikapo Juni, 2021.

- 80% ya jamii ishiriki kikamilifu katika usafi wa mazingira na kuboresha mazingira ili kupunguza magonjwa ya mlipuko ifikapo Juni, 2021.
- Jamii zote ziwezeshe kusaidia mtumishi wa afya kufanya huduma za wagonjwa wan nje ifikapo Juni, 2021.

Lengo D: Kuongeza Idadi na Ubora wa Huduma za Jamii na Miundombinu

Malengo Mahususi Yaliyopangwa

- Kilometa 465 za barabara kuboreshwa /kukarabatiwa ifikapo Juni, 2021.
- Madaraja 3 kujengwa na 3 kukarabatiwa ifikapo Juni, 2021
- Idadi ya majengo yaliyojengwa na samani katika mashule kuongezeka ifikapo Juni, 2021.
- Miundombinu za shule kuboreshwa ifikapo Juni, 2021
- Madaraja sita kujengwa / kukarabatiwa ifikapo juni, 2021
- Vijiji 26 visaidiwe kuwa na huduma ya maji safi na salama ifikapo juni, 2021.
- Miundombinu ya ofisi ya DMO kuboreshwa ifikapo Juni, 2021

Lengo E: Kuongeza Utawala Bora na Huduma za Kiutawala.

Malengo Mahususi Yaliyopangwa

- Ustawi wa jamii na gharama za uendeshaji kusimamiwa ifikapo Juni, 2021
- Idara ya fedha kubainisha gharama na matumizi yaliyofanyika ifikapo juni, 2021

- Kuandaa taarifa za fedha zilizokamilika kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka, na mwaka mzima ifikapo Juni, 2021.
- Idara ya fedha kusimamia gharama za kuendesha ofisi 36 ifikapo Juni, 2021.
- Kutoa mafunzo ya kitaaluma kwa watumishi wa idara ya fedha hadi, Juni, 2021.
- Kulipa madeni ya Halmashauri ifikapo Juni, 2021.
- Mapato ya ndani ya Halmashauri kuongezeka kutoka milioni 398 hadi 478 ifikapo Juni, 2021.
- Mikutano 80 ya bodi za zabuni na gharama za kuendesha ofisi 36 kusimamiwa ifikapo Juni, 2021.
- Kuzingatia utawala wa sharia katika ngazi zote za utawala katika Halmashauri ifikapo Juni, 2021.
- Idadi ya hoja za ukaguzi wa fedha kupungua kutoka 45 hadi 15 hadi Juni, 2021.
- Kusimamia stahiki za watumishi wa idara ya ukaguzi wa fedha na vifaa vya kufanyia kazi ifikapo Juni, 2021.
- Uelewa kuhusu stadi za usafi na usafi wa mazingira katika vijiji 4 kuboreshwa ifikapo Juni, 2021.
- Stahiki za madiwani 31, na watumishi 100 wa Halmashauri na gharama za uendeshaaji kusimamiwa ifika Juni, 2021.
- Kuimarisha rasilimali watu na vitu ili kutoa huduma bora ifikapo Juni, 2021

Lengo F: Kuimarisha Usimamizi wa Huduma za Dharula na Majanga

Malengo Mahususi Yaliyopangwa

- Vijiji 119 na kata 23 kutekeleza miradi ya maendeleo ifikapo Juni, 2021.
- Idadi ya biashara zenye leseni kuongezeka ifikapo Juni, 2021.
- Wajasiliamali wadogo kupewa elimu ya biashara na ujuzi ifikapo Juni, 2021
- Kusimamia maafisa biashara wa Wilaya, stahiki za watumishi wa ofisi, na gharama za uendeshaji wa ofisi ifikapo Juni, 2021.
- Vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS) kuongezeka kutoka 2 hadi 6, na kuongezeka kwa vyama vya ushirika wa masoko ya mazao ya kilimo ifikapo Juni, 2021.

Lengo G: Kuongeza Usimamizi Endelevu wa Maliasili na Mazingira ya Jamii

Malengo Mahususi Yaliyopangwa

- Kuongeza idadi ya mashamba yaliyopimwa kutoka 200 hadi 500 hadi Juni, 2021.
- Kuongeza idadi ya watu wenye hati milki za ardhi ifikapo Juni, 2021.
- Kuongeza uwezo wa Halmashauri katika kuwezesha, kukagua, na kufuatilia miradi kwa kuinua utambuzi na kuwajengea uwezo maafisa ifikapo Juni, 2021.
- Kata 5 kupata maji safi na salama ifikapo Juni, 2021.
- Kuongeza idadi ya vijiji vilivyo na mipango ya ardhi na hati miliki za kimila ifikapo Juni, 2021.

2.4 Uchambuzi wa Taasisi

Lengo la kuchambua hali halisi ya Halmashauri ni kuangalia utendaji wa kijamii na kiuchumiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ili

kuweza kufanya maamuzi ambayo yatasaidia kufanya maamuzi ambayo yatapelekea kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP). Kwa kutumia zana ya SWOC Halmashauri itagundua ubora, udhaifu, fursa na changamoto ambazo zitatoa mwongozo katika kubainisha mambo ya msingi ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi na serikali na jamii kwa ujumla.

MUUNDO WA JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SWOC

| Mambo muhimu | Uimara | udhaifu | fursa | Changamoto |
|---------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Kuwa na kilimo cha kisasa na cha kibiashara | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa ardhi yenye rutuba • Hali ya hewa nzuri kwa kilimo. | <ul style="list-style-type: none"> • Zana duni za kilimo na mashamba makubwa. • Kutokuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi. • Mvua zisizo tarajiwa | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa nguvu kazi. • Uwepo wa mashamba makubwa kama vile ya miwa. | <ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa mtaji, • Teknolojia duni • Upungufu wa masoko. • Kuwepo kwa wanyama pori katika makazi ya watu. |
| Kuimarisha miundo mbinu (barabara na ICT) | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa mtandao wa ICT • Uwepo wa mtandao barabara | <ul style="list-style-type: none"> • Ukarabati usioridhisha wa miundo mbinu mbalimbali | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa fedha za ujenzi wa barabara. | <ul style="list-style-type: none"> • upungufu wa fedha hasa katika uendeshaji wa ICT • fedha kidogo za maendeleo kutoka serikalini |
| Kukuza utalii | <ul style="list-style-type: none"> • Kuwa na maeneo | <ul style="list-style-type: none"> • Miundo mbinu | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa watalii wa | <ul style="list-style-type: none"> • Hakuna matangazo |

| Mambo muhimu | Uimara | udhaifu | fursa | Changamoto |
|-----------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| | ya kitalii | hafifu ya barabara <ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa watumishi | ndani na nan je. | <ul style="list-style-type: none"> • Ushirikiano mdogo kati ya Serikali kuu na Serikali za mitaa. |
| Kuboresha huduma za jamii (afya, maji na elimu) | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa vifaa tiba, shule na vyanzo vya maji. | <ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa waganga • Shortage of staff. | <ul style="list-style-type: none"> • Kiwango kidogo cha maambukizi. • Shule kufanya vizuri. • Uwepo wa zahanati 59 • Uwepo wa mabonde ya mito | <ul style="list-style-type: none"> • Kutokuwepo kwa mamlaka ya maji • Kukosekana kwa hospitali ya Halmashauri • Upungufu wa walimu wa sayansi |
| Maendeleo ya biashara kubwa na biashara ndogo ndogo | <ul style="list-style-type: none"> • Kutoa leseni za biashara kwa wakati. | <ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa taasisi za biashara ndogo ndogo • Upungufu wa elimu ya biashara. • Upungufu wa mitaji | <ul style="list-style-type: none"> • Utulivu wa kisiasa • Amani na usalama • Idadi kubwa na inayoongezeka ya watu • Uwepo wa viwanda vidogo. • Uwepo wa taasisi za fedha. | <ul style="list-style-type: none"> • Ugumu wa kufikika wa maeneo mengi ya Wilaya. • Pato dogo la kila mwanannchi wa kawaida |
| Usimami zi wa matumizi bora ya ardhi | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa maeneo yaliyopimwa | <ul style="list-style-type: none"> • Upungufu wa watumishi mfano wathamini na wapima ardhi | <ul style="list-style-type: none"> • Uwepo wa ardhi inayotakiwa kupimwa. | <ul style="list-style-type: none"> • Ukosefu wa vifaa vya kupimia ardhi. • Ukosefu wa mpango mji (master plan) |

| Mambo muhimu | Uimara | udhaifu | fursa | Changamoto |
|---------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| | | <ul style="list-style-type: none"> Kukosekana kwa mpango wa matumizi ya ardhi Migogoro ya ardhi | | |
| Usimami zi wa Misitu, ufugaji nyuki, na wanyama pori | <ul style="list-style-type: none"> Uwepo wa misitu Uwepo wa vichaka | <ul style="list-style-type: none"> Matumizi yasiyofaa ya rasilimali za misitu | <ul style="list-style-type: none"> Mahitaji makubwa ya mazao ya nyuki. | <ul style="list-style-type: none"> Uzalishaji usio wa kitaalamu Uanzishwaji wa moto |
| Kuondoa masuala mtambuka (VVU/ UKIMWI , majanga, mazingira, rushwa) | <ul style="list-style-type: none"> Uwepo wa miundombinu ya afya | Upungufu wa uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira, kujikinga na UKIMWI, na majanga mengine. | <ul style="list-style-type: none"> Ufahamu wa VVU na UKIMWI Ufahamu mdogo kuhusu rushwa, na uhifadhi wa mazingira na majanga. | <ul style="list-style-type: none"> Uharibifu wa mazingira Uchomaji wa misitu na vichaka |

| Mambo muhimu | Uimara | udhaifu | fursa | Changamoto |
|----------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
